HAKI ZAKO KAMA MFANYAKAZI:

- Uko na haki sawa sawa ya kazi kama mu Finlandais.
- Utapata salaire ya juu kama unapitisha saa zako za kawaida.
- Una haki ya kuwa na congé ya ugonjwa.
- Boss wako atakuambia kuhusu kazi yako.
- Unaweza jiunga mu groupe yenye itakusaidia ku mashauri kuhusu profit na haki yako mkazi kwenye unatumikia.
- Unaweza ambia boss wako matatizo yako yakazi ama kwa agent wa usalama na afya.
- Utalipiwa salaire kulingana na contrat ya bafanyakazi na ya maboss.

HAKIKISHA HAWAKUVURUGI KWA HIZI NJIA:

- Hauna contrat ya kazi.
- Haulipwi kulingana na contrat yako.
- Haulipi tax.
- Unabaguliwa kuhusu rangi yako au dini.
- Mtu hapashwi kutumika nafasi zenye haziko za muzuri wala nafasi zenye zinaweza kukuletea tatizo la afya.
- Unahitaji kulipa mtu kusudi upate kazi ama unasukumwa kufanya kazi yenye hautaki kufanya.

CONTRAT WA JUMLA = Contrat baina ya groupe ya bafanyakazi na mu groupe ya maboss. Hii contrat inasema watu wanatakiwa kutumika saa ngapi na kulipwa salaire ngapi.

MSIMAMIZI WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI = Wakala linalolenga kupunguza hatari za afya za mfanyakazi kazini.

UBAGUZI WA MFANYAKAZI = Ubaguzi wa mfanyakazi kazini juu ya nationalité, rangi au dini. Ubaguzi wa mfanyakazi haikubaliki na sheria ya Finlande.

GROUPE YA BAFANYAKAZI = Groupe la bafanyakazi inasimamia haki za bafanyakazi. Kila mtu anachagua mwenyewe kama anataka kijuinga na groupe hiyo. Groupe ziko nyingi inchini Finlande.

BIASHARA HARAMU YA KUUZA WANADAMU= Mfanyakazi anaweza kudanganywa au kubembelezwa kufanya kazi bila contrat ya kazi, kulipwa salaire ndogo zaidi, kulazimishwa kufanya masaa mengi ku kazi au kufanya kazi ili ulipe deni ya boss wako. Kutisha mfanyakazi ama familia yake ni biashara haramu ya kuuza wanadamu na inavunja haki za binadamu.

MAWASILIANO:

- Ofisi ya tax **vero.fi** na huduma ya cheti cha tax: **029497000**
- Agence Nationale Finlandaise pour l'Education **oph.fi**: **0295331000**
- Agent wa usalama na afya ku kazi: **0295016620**
- Groupe ya bafanyakazi inchini Finlande (SAK): **0800414004**
- Biashara haramu ya kuuza wanadamu: **0295463177**

IOM UN MIGRATION

UNATAFUTA KAZI?

HATUA ZA KWANZA ZA MKIMBIZI KUANZA MAISHA YA KAZI INCHINI FINLANDE

MASHAURI KUHUSU MAISHA YA MU FINLANDE:

- Fika kukazi mbele ya wakati.
- Heshimia saa za kazi na siku za mapumziko ambazo ulikubaliana kabla ya kuanza kazi.
- Fuatilia sheria za kazi yako.
- Usiogope kuuliza ushauri.
- Jishughulikishe mu kazi yako na uwe mfanyakazi wa kujitegemea.
- Fanya kazi yako kwa uangalifu.
- Ukigonjwa na kama hautafika kukazi, mjulishe boss wako haraka iwezekanavyo.
- Tunza afya yako na pumzika vizuri.
- Uvumilie kuzoea mazingira ya kazi sababu inaweza kukamata muda.

SWAHILI

KUJIANDAA KUFANYA KAZI

- Kama mkimbizi utakuwa umeshapata kibali cha kuishi na haki ya kufanya kazi ukifika Finlande.
- Unaweza kupata kazi kama unaongea kifinlandais au kisuédois. Ni muhimu kujifunza lugha!
- Elimu ni muhimu. Sehemu nyingi za kazi unahitaji vyeti / certficat ya elimu.
- Maboss mara nyingi wanaomba kuona vyeti/certificat yako ya elimu na kazi. Ni muhimu kugeuza vyeti/certificat yako mlugha ya kifinlandaise.
- Kama uko na grade yako na kama unapenda kuendelesha masomo, unaweza kuuliza wenye Agence Nationale Finlandaise pour l'Education **oph.fi** au bureau ya Valvira **valvira.fi**.
- Kuzuri upate kazi unahitajika ya kuwa na cheti / certificat ya busafi. Ukitaka kufanya kazi ya kujenga, unapashwa kuwa na certificat ya usalama kazini.
- Connaissance yako ya maisha mfinlande itakusaidia ukianza kufanya kazi. Kitabu kinachozungmumzia juu ya maisha ya Finlande unaweza kupata kwa hii address: **yhteiskuntaorientaatio.fi** kwa lugha ya kifinlandaise na kiingereza.

KUTAFUTA KAZI

- Ofisi yako ya Kazi (ofisi ya TE) inatosha ushauri kutafuta kazi na habari kuhusu kazi zinapatikana na masomo yenye inahusu wakimbizi kuweza kuishi Finlande. Habari zaidi: **te-palvelut.fi**
- Kama hauna kazi, uende ku TE-toimisto haraka iwezekanavyo kuwajulisha ili uweze kupokea mafao ya kukoza kazi.
- Kama umejisajili kama mtafutakazi ku TE-toimisto, ni lazima kuendelea kutafuta kazi kila wakati. Unapashwa kukubali masomo au kazi ambayo TE-toimisto itakupa.
- Kazi za mingi zinalombewa ku internet. Unaweza kujaza formulaire la kazi ku internet au kutuma CV yako kupitia e-mail address.
- Boss atachagula batafutakazi kwa mahojiano ya kazi. Jitayarishe kujibia juu ya nini utakuwa mfanyakazi mzuri kwa hiyo kazi. Kisha mahojiano na batafutakazi bengine atachagula mwenye anafikiri atakuwa mzuri.

KUANZA KAZI MPYA

- Kumbuka kutia signature ku contrat ya kazi na boss. Soma contrat yako vizuri mbele ya kutia signature juu uelewe kila kitu. Contrat itakuwa na habari zote kuhusu salaire, saa za kazi, kipindi ya contrat na programme yote ya kazi. Contrat haipashwi kuwa na habari yo yote ya bongo.
- Lazima ukuwe na compte ya banque juu ya kulipiwa salaire. Ambia boss wako kuhusu compte yako ya banque.
- Omba carte yako ya tax ku Bureau ya Tax ama unaweza kuitafuta kwenye internet: **omavero.fi**. Mpatie carte yako ya tax kwa boss wako juu wasikate tax ya 60% kutoka salaire yako. Onyesha numero zako za compte kwa Bureau ya Tax juu wakurudishie tax kama watakuwa na sababu.
- Uwe na contrat yako ya kazi kila wakati. Kama wanakulomba kuonyesha contrat yako ku ofisi ya KELA au bureau zingine, unaweza kuphotocopier.
- Kama weye ama mfamilia yako kuko mtu anapokea msaada wa KELA au bureau zingine, ni lazima kujulisha moja kwa moja mbele ya kuanza kazi yako. Ni mzuri kuwajulisha kwa kuwaonyesha karatasi au kupeleka contrat yako.